BENKI KUU YA TANZANIA



# TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

Aprili 2026

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia....................1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa....................5
2.1 Uchumi wa Ndani....................5
2.2 Mfumuko wa Ndai....................5
2.3 Sera ya Fedha....................8
2.4 Viwango vya Fedha....................10
2.5 Masoko ya Fedha....................10
2.6 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali....................12
2.7 Mwenendo wa Deni la Taifa....................13
2.8 Mwenendo wa Sekta ya Nje....................15
3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar....................18
3.1 Mfumuko wa Bei....................18
3.2 Bajeti ya Serikali....................18
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje....................19
Viambatisho....................21
Tafsiri ya dhana Muhimu....................34

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026, unatarajiwa kuendelea kuwa imara lakini kwa mwelekeo wa kupungua. Shirika la Fedha la Kimataifa lilitoa taarifa ya maoteo ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwezi Aprili mwaka 2026 ikionesha kupungua hadi kufikia asimilia 3.1 ikilinganishwa na maoteo ya asimilia 3.3 yaliotolewa na taarifa hiyo ya mwezi Januari 2026. Taarifa hiyo inaonesha kuwa, mwendendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia umeathiriwa na ongezeko la hali ya kutotabirika inayotokana na migogoro ya kijiopolitiki, hususan katika eneo la Mashariki ya Kati (Kielelezo 1.1a na Kielelezo1.1b).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Shirika la Fedha la Kimataifa, maoteo ya ukuaji kwa nchi zilizoendelea umeendelea kuwa sawa na maoteo ya mwezi Januari 2026, wakati maoteo ya ukuaji katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea umepungua, isipokuwa India. India, inatarajiwa kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji, ukichangiwa na kuimarika kwa mahitaji ya ndani pamoja na matarajio ya mauzo ya nje kufuatia Marekani kupunguza ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazotoka nchini humo (Jedwali 1.1). Wastani wa ukuaji kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, unatarjiwa kufikia asilimia 4.3, ikiwa ni maoteo ya chini ikilinganishwa asimilia 4.6 iliyotabiriwa mwezi Januari 2026. Hali hii imechangiwa na kuongezeka kwa vichocheo vya mfumuko wa bei, hususan gharama za mbolea na usafirishaji majini kulikosababishwa na mvurugiko wa mnyororo wa ugavi Mashariki ya kati.

**Jedwali 1.1: Ukuaji wa Uchumi Dunia**

| | 2023 | 2024 | 2025 | 2026[r] | 2027[p] |
|---|---|---|---|---|---|
| **Dunia** | 3.5 | 3.3 | 3.4 | 3.1 | 3.2 |
| Nchi zilizoendelea | 1.7 | 1.8 | 1.9 | 1.8 | 1.7 |
| Marekani | 2.9 | 2.8 | 2.1 | 2.3 | 2.1 |
| Eneo la Ero | 0.4 | 0.9 | 1.4 | 1.1 | 1.2 |
| Uingereza | 0.3 | 1.1 | 1.3 | 0.8 | 1.3 |
| Japani | 0.7 | -0.2 | 1.2 | 0.7 | 0.6 |
| **Nchi zinazoibukia na Zinazoendelea** | 4.7 | 4.3 | 4.4 | 3.9 | 4.2 |
| Brazili | 3.2 | 3.4 | 2.3 | 1.9 | 2.0 |
| Urusi | 4.1 | 4.9 | 1.0 | 1.1 | 1.1 |
| India | 7.2 | 7.1 | 7.6 | 6.5 | 6.5 |
| Uchina | 5.4 | 5.0 | 5.0 | 4.4 | 4.0 |
| **Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara** | 3.8 | 4.2 | 4.5 | 4.3 | 4.4 |

Chanzo: IMF-World Economic Outlook Database April 2026
Tanbihi: p inaonesha makadirio ya ukuaji wa awali

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Bei za bidhaa kwa mwezi Machi 2026 zilionesha mwenendo mchanganyiko lakini kwa ujumla zilikuwa na mwelekeo wa kuongezeka. Bei ya mafuta ghafi ilifikia wastani wa dola za Marekani 95.58 kwa pipa, kutoka dola za Marekani 68.01 kwa pipa mwezi Februari 2026, hali iliyochochewa na kuongezeka kwa mvutano wa migogoro Mashariki ya Kati. Kwa upande mwingine, bei ya dhahabu iliendelea kubadilika kwa wastani, ikipungua hadi

dola za Marekani 4,855.54 kwa wakia moja kutoka dola za Marekani 5,019.97 mwezi uliotangulia, ikichangiwa na matarajio ya mabadiliko ya sera ya fedha ya Benki Kuu ya Marekani (Federal Reserve), ambayo yalisababisha kuimarika kwa thamani ya dola ya Marekan, na kupunguza mahitaji ya dhahabu kama mali salama.

Kwa kiasi kikubwa, bei za bidhaa za kilimo zilionesha mwelekeo mchanganyiko, zikiakisi mvurugiko wa mnyororo wa ugavi Mashariki ya Kati na mabadiliko ya uzalishaji. Bei ya kahawa aina ya Robusta ilipungua kufuatia ugavi wa kutosha katika soko la dunia. Kwa upande mwingine, bei ya kahawa aina ya Arabika, sukari na mafuta ya mawese zilipanda, zikisababishwa na kuongezeka kwa bei ya mafuta ghafi illiyoongeza gharama za usafirishaji pamoja na kuchochea mahitaji ya nishati mbadala (biofuels). Vilevile, bei za ngano na pamba ziliongezeka kutokana hali mbaya ya hewa nchini Marekani na Australia. Bei ya mbolea, hususan Urea na DAP, ilipanda pia ikiakisi zuio la uuzwaji nje wa mbolea kutoka nchini China pamoja na mvurugiko wa ugavi kwenye Mlango-Bahari wa Hormuz. Sababu hizi kwa pamoja zimesababisha changamoto za ugavi kwa baadhi ya nchi kuelekea kwenye misimu kilimo (Kielelezo 1.2).

**Kielelezo 1.2: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

Mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi zilizoendelea, hususan Marekani na eneo la Euro, likichangiwa na kutokuwa na utulivu wa masoko ya nishati kufuatia misukosuko katika Ghuba ya Uajemi. Mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi ulikuwa mchanganyiko. Nchini China, kasi ya mfumuko wa bei ilipungua kufuatia hatua ya Serikali kudhibiti bei za mafuta ya ndani, wakati India na Brazil zilishuhudia ongezeko la mfumuko wa bei uliotokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya mali, na kupanda kwa gharama za pembejeo za kilimo, mtawalia. Mfumuko wa bei kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara uliendelea kubaki ndani ya wigo unaokubaliwa. Hata hivyo, ongezeko la hivi karibuni la bei za mafuta katika soko la dunia linaashiria hatari kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa kipindi kijacho (Kielelezo 1.3, Kielelezo 1.4, na Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.5: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

**Kisanduku 1: Mgogoro Katika Mlango Bahari wa Hormuz: Athari kwa Uchumi wa Tanzania.**

Mlango Bahari wa Hormuz, ni njia nyembamba ya bahari inayotenganisha Iran na Oman, na ni njia muhimu duniani kwa biashara ya nishati. Kila siku, takribani mapipa milioni 21 ya mafuta ghafi hupita katika njia hii yenye upana wa kilomita 33, takriban moja ya tano ya matumizi yote ya mafuta duniani. Mzozo wa kijeshi kati ya Marekani–Israel na Iran uliposababisha kufungwa kwa njia hii mwezi Machi 2026, athari kwa masoko ya kimataifa ya nishati zilikuwa za haraka na kubwa.

Kufungwa kwa Mlango wa Hormuz hakuishoii tu kwenye usambazaji wa mafuta ghafi. Mlango huo pia ni njia kuu ya usafirishaji kwa nchi za Ghuba zinazozalisha mbolea, ambazo huchangia takriban nusu ya uzalishaji wa kimataifa wa salfa, robo ya uzalishaji wa amonia, na theluthi moja ya mauzo ya nje ya urea (GSA, 2026). Ndani ya juma la kwanza la mzozo, bei ya mbolea za nitrojeni ilipanda kwa asilimia 30 hadi 40, huku bei ya urea ikiongezeka kwa asilimia 43 (Reuters, 5 Machi 2026).

Viwango vya usafirishaji wa makasha kati ya Asia na Afrika pia vimeongezeka hadi wastani wa dola za Marekani 4,800 kwa kasha la futi 40, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mara mbili ya kiwango cha dola 2,000 kilichokuwepo mwanzoni mwa mwaka 2025 (Drewry World Container Index, Machi 2026; Freightos Baltic Index, 2026). Kwa nchi zinazotegemea kwa kiasi kikubwa uagizaji wa nishati, chakula, na bidhaa za viwandani, ongezeko hili la ghafla lilisababisha mfumuko mkubwa wa bei. Ongezeko la pamoja la gharama za usafirishaji, bidhaa, na nishati kunasababisha mshtuko wa ugavi kupitia njia mbalimbali, na athari kwenye mfumuko wa bei, urari wa malipo, na uimara wa jumla wa uchumi.

Mshtuko huo unasambaa katika uchumi wa ndani kwa njia mbili zinazoendana. Njia ya kwanza ni kupitia gharama za moja kwa moja za nishati. Bei ya mafuta ghafi inapopanda katika soko la dunia, gharama za uagizaji wa bidhaa za petroli huongezeka. Njia ya pili ni kupitia gharama za usafirishaji na usambazaji. Masoko ya bidhaa za ndani hutegemea zaidi barabara kusafirisha mazao, vifaa vya ujenzi, na bidhaa za matumizi kutoka bandarini na mashambani kwenda kwenye masoko nchini. Hivyo, bei kubwa ya mafuta huongeza gharama za usafirishaji na usambazaji wa mizigo. Hatimaye, gharama hizi huhamishwa kwa mlaji wa mwisho kupitia ongezeko la bei za vyakula, saruji, mbolea, na bidhaa nyingine za kaya sokoni.

Kidunia, usalama wa chakula unabakia kuwa suala lenye umuhimu zaidi. Nchi nyingi za Afrika zinazopakana na Bahari ya Hindi hupata kati ya asilimia 30 hadi 50 ya mbolea zinazozalishwa na nchi za Ghuba (GSA, 2026). Kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi kunakoendelea sambamba na bei ya mbolea iliyoongezeka duniani,ambayo imeunganishwa na kupanda kwa gharama za usambazaji, inapunguza uwezo wa wakulima kugharamia upandaji,

umwagiliaji, na usafirishaji wa mazao, hivyo kuongeza hatari ya kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei za vyakula nchini. Ongezeko hili linajidhirisha zaidi kupitia viwango vya kubadilisha fedha. Kadri ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta zinavyoongeza mahitaji ya fedha za kigeni, ndivyo huweka shinikizo la kushuka thamani ya shilingi na kuongeza kwa gharama kwa bidhaa mbalimbali kutoka nje zaidi ya mafuta. Mzigo huo hatimaye huwa mkubwa zaidi kwa kaya za kipato cha chini ambazo hutumia sehemu kubwa zaidi ya kipato chao katika nishati, usafiri, na chakula. Athari za kibajeti zinaweza kutokea ikiwa Serikali itaingilia kusaidia kaya kupitia ruzuku kukabiliana na hali hiyo.

Athari za kisekta zinatofautiana. Sekta ambazo zinategemea mafuta zaidi na zenye uwezo mdogo wa kupanga bei, kama vile usafirishaji wa kibiashara, huduma za kiutawala na saidizi, zinakabiliwa na shinikizo endelevu la kupungua kwa faida na hatari ya kupoteza wateja kutokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji. Mikopo ya mabenki kwenda sekta ya kilimo inaweza pia kupungua, jambo litakalopunguza uwezo wa wakulima kununua pembejeo na kuongeza zaidi shinikizo la bei za chakula kutokana na kupungua kwa uzalishaji badala ya usambazaji pekee. Kinyume chake, mshtuko huo unaweza kuharakisha mabadiliko ya kimuundo yanayonufaisha sekta nyingine. Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inaweza kunufaika kadri kaya na biashara zinavyohamia zaidi kwenye biashara mtandao, malipo ya kielektroniki, na mawasiliano ya mtandaoni pindi gharama za miamala ya fedha taslimu zinapoongezeka, ilhali huduma za kifedha na bima zinaweza kukua kadri ukuaji wa mahitaji ya kujikinga, ufadhili wa biashara pamoja na nyenzo za kudhibiti hatari zinavyoongezeka.

Kwa vitendo, hii ina maana kwamba wakati bei za mafuta dunia zinapopanda, mapato ya mauzo ya nje ya dhahabu huongezeka kwa kiwango cha kutosha kufidia gharama kubwa za uagizaji wa mafuta, hivyo kupunguza athari hasi kwenye urari wa akaunti ya sasa.

Kinachoitofautisha Tanzania na chumi nyingi zinazofanana nayo ni sifa ya kimuundo inayofanya kazi kama kimbilio la asili wakati wa mtikisiko wa bei za bidhaa duniani. Mauzo ya dhahabu huchangia kati ya asilimia 30 hadi 40 ya mapato yote ya fedha za kigeni, huku thamani ya mauzo hayo yakizidi dola za Marekani bilioni 3 kwa mwaka unaoishia Machi 2026. Kihistoria, bei za mafuta na dhahabu huongezeka kwa mwelekeo mmoja wakati wa migogoro ya kijiografia ya kisiasa kutokana na vihatarishi vinavyofanana, matumizi ya dola ya Marekani, na ongezeko la mahitaji ya uwekezaji salama (Baur & Lucey, 2010; IMF, 2024). Hii in amaana kwamba wakati bei za mafuta duniani zinapopanda, mapato ya mauzo ya dhahabu nje huongezeka kiwango kufidia ongezeko la gharama za uagizaji mafuta, na hivyo kusaidia kuboresha urari wa malipo wa kawaida. Hata hivyo, hali hii haiondoi kabisa mzigo wa ongezeko la gharama za mafuta kwa soko la ndani. Kaya na biashara zinaendelea kugharamika zaidi kwenye petroli na dizeli. Katika uchumi mpana, mapato ya dhahabu yanaipa Tanzania uwezo wa kustahimili mishtuko ambayo nchi jirani hazina.

Pamoja na kinga ya dhahabu, mfumo wa sera ya fedha umeundwa mahsusi kuwezesha uchumi kuhimili mishtuko ya bei ya bidhaa kutoka nje bila kusababisha mfumuko mkubwa wa bei. Taarifa ya Maoteo ya Ukuaji wa Uchumi wa Dunia toleo la Aprili 2026 iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) inaonesha kuwa mishtuko ya kisiasa duniani huongeza wastani wa bei duniani kwa takribani asilimia 2.5 katika kipindi cha miaka mitatu. Uzoefu wa Tanzania umeonesha ongezeko dogo zaidi ikilinganishwa na wastani wa dunia, kwa sehemu, ikitokana na mfumo wa EWURA wa kupanga bei kwa uwazi na kwa kuzingatia gharama halisi za soko, jambo linalosaidia kudhibiti wa mfumuko wa bei.

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Uchumi wa Ndani

Uchumi uliendelea kuwa imara katika robo ya nne ya mwaka 2025, ukikua kwa asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 5.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.1a). Ukuaji huo ulikuwa kwa sekta mbalimbali, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za kilimo, huduma za kifedha na bima, pamoja na ujenzi (Kielelezo 2.1b).

Kwa kuzingatia viashiria vya mara kwa mara vya kiuchumi, pamoja na athari za mvutano wa Mashariki ya Kati, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026 na asilimia 6.1 robo inayofuata. Mwenendo huo unachangiwa na kuimarika kwa shughuli za ujenzi, kilimo, pamoja na huduma za kifedha na bima.

**Kielelezo 2.1a: Ukuaji wa Uchumi kwa Robo Mwaka**

Asilimia




Chanzo: Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Kielelezo 2.1b: Mchango wa Baadhi ya Sekta Katika Pato la Taifa Kwa Robo Mwaka**




Chanzo: Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## 2.2 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa wa chini, thabiti, ndani ya lengo la kitaifa na vigezo vya mtangamano wa kikanda (SADC na EAC). Kwa mwezi Machi 2026, mfumuko wa bei ulikua asilimia 3.2, sawa na mwezi uliotangulia (Jedwali 2.2.1 na Kielelezo 2.2.1). Katika kipindi kifupi kijacho mwenendo wa mfumuko wa bei unatarajiwa kuchangiwa zaidi na vihatarishi vinavyotokana na mgogoro wa Mashariki ya kati. Hata vivyo, kuimarika kwa hali ya ndani, kama vile chakula cha kutosha, uimara wa sarafu, pamoja na sera thabiti ya fedha zinatarajiwa kwa kiasi flani kufidia athari za nje (hususan, bei kubwa za mafuta na mbolea) kwenye mfumuko wa bei wa jumla. Kwa kuzingatia sababu hizi, Benki inatarajia mfumuko wa bei kubakia ndani ya wigo wa asilimia 3-5 kwa kipindi chote cha mwaka 2026.

## Jedwali 2.2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

| | | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Mac-26 | Feb-26 | Mac-26 | Mac-26 | Feb-26 | Mac-26 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 1.9 | 1.2 | 1.8 | 5.4 | 5.7 | 5.5 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 3.5 | 2.1 | 2.1 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.2 | 0.0 | 0.5 | 2.0 | 1.1 | 1.3 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.9 | 0.4 | 0.7 | 3.8 | 1.7 | 1.6 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 0.3 | 0.0 | 0.1 | 2.2 | 2.5 | 2.3 |
| Afya | 2.5 | 0.2 | 0.0 | 0.4 | 1.4 | 0.9 | 1.1 |
| Usafiri | 14.1 | 0.4 | 0.1 | 0.5 | 2.1 | 4.0 | 4.2 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.1 | 0.2 | 0.0 | 0.1 | 1.1 | 1.0 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 1.6 | 0.6 | 0.6 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 0.1 | 0.6 | 4.1 | 0.3 | 0.9 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.1 | 0.6 | 0.4 | 1.7 | 1.7 | 2.1 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.7 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.2 | 0.0 | 0.3 | 3.3 | 3.2 | 3.3 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | 0.8 | 0.5 | 0.8 | 3.3 | 3.2 | 3.2 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.2 | 0.1 | 0.3 | 2.2 | 2.1 | 2.2 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | 2.5 | 1.4 | 2.3 | 6.0 | 5.9 | 5.6 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | 2.8 | 0.5 | 2.1 | 7.9 | 2.8 | 2.1 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | 0.1 | 0.2 | 0.3 | 1.0 | 2.2 | 2.4 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 1.2 | 0.6 | 1.2 | 4.5 | 3.7 | 3.6 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 0.1 | 0.1 | 0.5 | 4.0 | 0.3 | 0.7 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.4 | 0.2 | 0.4 | 2.3 | 2.1 | 2.1 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 2.2.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi, ambao haujumuishi bidhaa za chakula zisizosindikwa na nishati, uliongezeka na kufikia asilimia 2.2 mwezi Machi 2026, kutoka asilimia 2.1 mwezi uliopita (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Hata hivyo kwa kipindi kifupi, mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi unaweza kuongezeka kidogo kutokana na changamoto za mnyororo wa ugavi unaohusiana na mgogoro wa Mashariki ya Kati.

## Kielelezo 2.2.3: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei ya vyakula kwa mwaka ulikuwa asilimia 5.5 mwezi Machi 2026, ukiwa chini kidogo ya asilimia 5.7 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.4a, Kielelezo 2.2.4b na Jedwali 2.2.1). Hali hii inaendana na kuimarika kwa uwepo wa chakula kutokana na matarajio ya uwepo wa kuongezeka kwa mavuno katika maeneo mengi nchini. Mfumuko wa bei ya chakula unatarajiwa kuendelea kupungua.

## Kielelezo 2.2.4: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao

a. **Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

### b. Mazao ya Vyakula Mbadala

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ilikuwa tani 533,634 mwishoni mwa mwezi Machi 2026, ikilinganishwa na tani 560,008 zilizorekodiwa mwezi uliotangulia. Kupungua kwa akiba ya chakula kulitokana na mauzo ya tani 26,374 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara mbalimbali katika kipindi cha mwezi huo, hatua iliyolenga kuleta utulivu wa bei za rejareja (Jedwali 2.2.2).

**Jedwali 2.2.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 | 567,469 |
| Feb | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 | 560,008 |
| Mac | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 | 533,634 |
| Apr | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 | |
| Mei | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 | |
| Jun | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 | |
| Jul | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 | |
| Ago | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 | |
| Sep | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 | |
| Okt | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 | |
| Nov | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 | |
| Des | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei za nishati, mafuta, na huduma za msingi ulipungua na kufikia asilimia 2.1 mwezi Machi 2026, kutoka asilimia 2.8 mwezi uliotangulia, ukiwa chini ya asilimia 7.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kupungua huku kulichochewa zaidi na kushuka kwa bei za mkaa na kuni. Wakati huohuo, bei za rejareja za petroli, dizeli, na mafuta ya taa ziliongezeka kidogo kutokana na ongezeko kubwa la bei za bidhaa za mafuta soko la dunia (Kielelezo 2.2.5 na Jedwali 2.2.1).

Mfumuko wa bei za bidhaa za msingi umeendelea kuwa na mchango mkubwa katika mfumuko wa bei wa jumla, ambapo kwa mwezi Machi 2026, ulichangia asilimia 1.7 sawa na mchango uliorekodiwa mwezi kama huo 2025 (Kielelezo 2.2.6).

**Kielelezo 2.2.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

**Kielelezo 2.2.6: Mchango Katika Mfumuko wa Bei**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## 2.3 Sera ya Fedha

Katika kikao chake kilichofanyika mwezi Aprili 2026, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), iliamua Kiwango cha Riba cha Benki Kuu (CBR) kubaki asilimia 5.75 kwa robo ya pili ya mwaka 2026. Uamuzi huu unaashiria mwelekeo wa tahadhari wa sera ya fedha ya kuwianisha vihatarishi katika mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi, kufuatia kuongezeka kwa hali ya kutokuwa na uhakika katika uchumi wa dunia. Kwa namna ya pekee, kuongezeka kwa mvutano Mashariki ya Kati unaendelea kudhoofisha biashara, uwekezaji, na utulivu wa uchumi duniani. Katika kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha, Kamati ya Sera ya Fedha pia ilipunguza wigo wa riba ya Benki Kuu kutoka pointi ± 200 hadi pointi ±150 kuanzia mwezi Aprili 2026. Sanjari na uamuzi huu, utekelezaji wa sera ya fedha utalenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa asilimia 1.5 juu au chini ya riba ya Benki Kuu "CBR".

Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwezi Machi 2026 uliendana na matarajio, licha ya changamoto zilizojitokeza duniani kufuatia ongezeko la mivutano ya kijiopolitiki. Kiwango cha ukwasi katika soko la fedha baina ya benki kiliendelea kuwa cha kutosha, huku riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki ikibaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu "CBR" (Kielelezo 2.3.1). Mwenendo huu ulidhihirishwa zaidi na kuendelea kupungua kwa mikopo ya muda mfupi kutoka Benki Kuu, "reverse repo", kwenda kwa benki za biashara, kutoka shilingi bilioni 581.4 hadi shilingi bilioni 430.8 katika kipindi cha mwezi wa mapitio (Kielelezo 2.3.2).

**Kielelezo 2.3.1: Riba ya Benki Kuu naWastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.3.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha uliendelea kukua sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa na ukuaji wa asilimia 23.2 mwezi Machi 2026, chini kidogo ikilinganishwa na asilimia 24.5 mwezi Februari 2026. Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuchangia sehemu kubwa ya ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3), ikikua kwa asilimia 24.1 katika mwaka ulioishia Machi 2026, ikiwa ni karibu na asilimia 24.4 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.3.3, Kielezo 2.3. 4, Kielelezo 2.3.5 na Jedwali 2.3.1).

### Kielelezo 2.3.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Jedwali 2.3.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| Kipengele | Kiasi (Shilingi Bilioni) Mac-25 | Feb-26 | Mac-26 | Ukuaji kwa mwaka (%) Mac-25 | Feb-26 | Mac-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 15,442.1 | 15,749.5 | 15,245.6 | 32.7 | 7.1 | -1.3 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 13,217.7 | 14,089.2 | 13,916.0 | 10.3 | 8.2 | 5.3 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 2,224.4 | 1,660.3 | 1,329.6 | --- | -1.5 | -40.2 |
| Rasilimali halisi za ndani | 36,699.8 | 47,319.8 | 49,001.1 | 11.6 | 31.7 | 33.5 |
| Madai rasmi ya ndani | 50,109.3 | 58,896.1 | 59,877.3 | 13.3 | 20.6 | 19.5 |
| Amana za Serikali zilizopo Ben | 8,039.9 | 9,956.8 | 10,272.1 | -5.6 | 24.7 | 27.8 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 37,999.3 | 46,054.2 | 47,216.5 | 14.0 | 24.5 | 24.3 |
| Rasilimali nyinginezo | -13,409.5 | -11,576.2 | -10,876.3 | 18.4 | -10.2 | -18.9 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 52,141.9 | 63,069.3 | 64,246.7 | 17.1 | 24.5 | 23.2 |
| Amana za fedha za kigeni | 13,605.9 | 14,569.7 | 14,998.4 | 30.9 | 13.7 | 10.2 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 38,536.0 | 48,499.6 | 49,248.3 | 12.9 | 28.2 | 27.8 |
| Amana zinginezo | 14,994.3 | 18,541.9 | 19,071.4 | 13.0 | 26.0 | 27.2 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 23,541.7 | 29,957.7 | 30,176.9 | 12.8 | 29.6 | 28.2 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 7,190.0 | 8,151.8 | 8,078.3 | 13.7 | 17.2 | 12.4 |
| Amana za hundi | 16,351.7 | 21,805.9 | 22,098.5 | 12.5 | 34.9 | 35.1 |
| Fedha za msingi (M0) | 11,793.1 | 14,990.0 | 14,998.9 | 15.8 | 24.1 | 27.2 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.3.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.3.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Ukuaji wa mikopo uliendelea kuwa imara katika shughuli zote muhimu, ambapo shughuli za uchimbaji madini zilirekodi ongezeko kubwa zaidi kwa asilimia 78.4, ikifuatiwa na biashara, uchukuzi na mawasiliano (Jedwali 2.3.2). Ukuaji wa mikopo katika shughuli za madini unaakisi jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali za kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo.

Kwa mgawanyo wa mikopo, mikopo kwa shughuli binafsi iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote ikiwa na asilimia 35.3, ikifuatiwa na biashara na kilimo (Kielelezo 2.3.6).

### Jedwali 2.3.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

| | Mac-25 | Jun-25 | Sept-25 | Des-25 | Jan-26 | Feb-26 | Mac-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | -24.8 | 20.8 | 32.4 | 91.1 | 91.4 | 103.9 | 78.4 |
| Biashara | 12.7 | 21.3 | 24.8 | 49.7 | 50.0 | 48.7 | 43.3 |
| Kilimo | 22.4 | 25.7 | 17.4 | 29.4 | 34.2 | 39.4 | 39.5 |
| Ujenzi | 36.3 | 30.2 | 27.6 | 28.9 | 27.9 | 31.9 | 28.5 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 35.1 | 25.7 | 15.7 | 25.6 | 29.5 | 28.1 | 21.8 |
| Hoteli na migahawa | 9.4 | 13.7 | 14.7 | 17.7 | 17.8 | 18.9 | 20.7 |
| Shughuli binafsi | 5.4 | 22.5 | 16.3 | 2.5 | 1.6 | 5.2 | 4.4 |
| Viwanda | 10.9 | 2.5 | 0.1 | -8.2 | -7.7 | -8.5 | -4.9 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

**Kielelezo 2.3.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.4 Viwango vya Riba

Mwezi Machi 2026, viwango vya riba za benki havikuwa na mabadiliko makubwa ikilinganishwa na mwezi uliotangulia. Wastani wa riba za mikopo ulibaki kuwa asilimia 15.11, huku riba za mikopo kwa wateja wakubwa (negotiated lending rates) zikiendelea kuwa takriban asilimia 12. Kutobadilika kwa viwango vya riba za mikopo kunaonesha kuwa mabadiliko ya sera ya fedha hayaathiri kwa haraka masharti ya mikopo ya rejareja.

Kwa upande wa amana, viwango vya riba kwa kiasi kikubwa havikuwa na mabadiliko, wakati riba za amana kwa wateja wakubwa ziliongezeka hadi asilimia 11.57 kutoka asilimia 11.48. Wigo kati ya riba za mikopo na ya muda mfupi uliongezeka hadi asilimia 5.85, kutoka asilimia 5.59 mwezi Februari 2026 (Jedwali 2.4.1).

**Jedwali 2.4.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa na Benki za Biashara**

Asilimia

| | Mac-25 | Jun-25 | Sept-25 | Des-25 | Feb-26 | Mac-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.86 | 2.90 | 2.92 | 3.02 | 2.98 | 2.89 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.50 | 15.23 | 15.18 | 15.24 | 15.11 | 15.11 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.83 | 15.69 | 15.52 | 15.46 | 15.41 | 15.45 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.94 | 12.68 | 12.84 | 12.38 | 12.19 | 12.21 |
| Riba za amana -jumla | 8.00 | 8.74 | 8.50 | 8.36 | 8.32 | 8.33 |
| Riba za amana (miezi 12) | 8.14 | 9.79 | 9.84 | 9.58 | 9.82 | 9.60 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.35 | 11.21 | 11.05 | 11.66 | 11.48 | 11.57 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 7.69 | 5.90 | 5.69 | 5.88 | 5.59 | 5.85 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.5 Masoko ya Fedha

### Soko la dhamana za Serikali

Mwenendo wa soko la fedha kwa mwezi Machi 2026, kwa kiasi kikubwa lilikuwa sambamba na sera ya fedha na uwepo wa ukwasi wa kutosha. Soko la dhamana za Serikali liliendelea kuwa imara, ambapo minada iliendelea kuwa na uhitaji mkubwa kuliko ilivyotarajiwa, ikiashiria uhitaji endelevu kutoka kwa wawekezaji unaochangiwa na hali ya utulivu wa uchumi.

Benki ilifanya minada miwili ya dhamana za Serikali ya muda mfupi yenye thamani ya shilingi bilioni 452.1 kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali na utekelezaji wa sera ya fedha. Minada hii ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 812.9 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 422 kilikubaliwa. Wastani wa riba ya dhamana za Serikali za muda mfupi ulipungua hadi asilimia 5.21 kutoka asilimia 5.68 iliyorekodiwa mwezi uliopita (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Wakati huohuo, minada ya hati fungani za miaka 2 na 20 yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 355.4 ilifanyika kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali. Minada hii ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 1,803.9, ambapo zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 344.1 zilikubaliwa. Hivyo, riba za hati fungani za miaka 2 na 20 ziliendelea kupungua hadi asilimia 8.36 na asilimia 10.71, mtawalia.

## Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya benki (IBCM) liliendelea kufanya kazi kwa ufanisi kwa mwezi Machi 2026, likiendelea kuwezesha ukwasi baina ya mabenki. Jumla ya mauzo katika soko ilipungua hadi shilingi bilioni 2,699.5 kutoka shilingi bilioni 2,796.5 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia, ambapo mikopo ya siku saba ilichukua takriban asilimia 60.7 ya mikopo yote (Kielelezo 2.5.2). Sambamba na uwepo wa ukwasi wa kutosha, wastani wa riba katika soko hili ulipungua kidogo hadi asilimia 6.32 kutoka asilimia 6.34 iliyorekodiwa mwezi Februari 2026, ikiendelea kuendana kwa karibu na riba ya Benki Kuu.

**Kielelezo 2.5.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha za kigeni

Mwezi Machi 2026, mahitaji ya fedha za kigeni baina ya benki katika soko yalipungua, hali inayoashiria uwepo wa ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni, kutokana na mauzo nje ya nchi, hususan dhahabu. Jumla ya miamala katika soko ilifikia dola za Marekani milioni 137.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 184.9 zilizouzwa mwezi uliotangulia, huku Benki Kuu ikipunguza mauzo yake kwa takribani nusu ya kiwango kilichouzwa mwezi uliotangulia hadi Dola milioni 65 kutoka Dola milioni 128.8 (Kielelezo 2.5.3).

Ndani ya mwezi huo, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa shilingi 2,583.23, ikilinganishwa na shilingi 2,650.24 kwa Dola moja ya Marekani katika mwezi kama huo mwaka 2025, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi kwa asilimia 2.52 kwa mwaka.

**Kielelezo 2.5.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2. 6 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Makusanyo ya mapato ya ndani mwezi Februari 2026 yaliendelea kuwa ya kuridhisha, yakifikia shilingi bilioni 2,972.9, juu ya lengo kwa asilimia 3.2. Serikali kuu ilikusanya shilingi bilioni 2,841.0, ikiwa juu ya lengo kwa asilimia 3.2, huku mapato yaliyosalia yakitokana na mamlaka za serikali za mitaa kupitia vyanzo vyao vya ndani.

Mapato ya kodi yalikuwa imara zaidi na kufikia shilingi bilioni 2,417.4, sawa na ongezeko la asilimia 5.7 juu ya lengo, ikiashiria athari chanya za maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi na uzingatiaji wa ulipaji kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 423.6, ikiwa ni asilimia 9 chini ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 465.7 (Kielelezo 2.6.1).

**Kielelezo 2.6.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Februari**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato, ambapo matumizi yalifikia shilingi bilioni 3,550.1. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 2,429.7 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 1,120.4 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.6.2).

**Kielelezo 2.6.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Februari**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

## 2.7 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) mwishoni mwa mwezi Machi 2026, lilifikia dola za Marekani milioni 50,457.5 likipungua kwa asilimia 1.2 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa mwezi uliopita. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70.4 ilikuwa ni deni la nje (Kiambatisho, Jedwali A10).

### Deni la Nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) lilipungua kwa asilimia 0.8 na kufikia dola za Marekani milioni 35,540.2 mwishoni mwa Machi 2026. Katika kiasi hicho, asilimia 82.7 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.7.1). Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Machi 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 70.3, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 103.7 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 48.0 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji kwa kiasi kikubwa haukuwa na mabadiliko, huku Mashirika ya kifedha ya kimataifa yakiendelea kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 57.8, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.7.2). Mikopo kwa ajili ya urari wa malipo ya nje na bajeti (BoP na budget support) iliongoza kwa kiasi kilichopokelewa ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66.7, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Euro) (Jedwali 2.7.3 na Jedwali 2.7.4).

**Jedwali 2.7.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopaji | Mac-25 Kiasi | Mac-25 Mchango (%) | Feb-26[r] Kiasi | Feb-26[r] Mchango (%) | Mac-26[p] Kiasi | Mac-26[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | 26,789.5 | 80.5 | 29,684.8 | 82.9 | 29,398.5 | 82.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 26,712.0 | 80.3 | 29,604.6 | 82.6 | 29,318.6 | 82.5 |
| Malimbikizo ya riba | 77.5 | 0.2 | 80.2 | 0.2 | 80.0 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,491.0 | 19.5 | 6,139.9 | 17.1 | 6,141.7 | 17.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,912.1 | 17.8 | 5,738.4 | 16.0 | 5,723.0 | 16.1 |
| Malimbikizo ya riba | 578.9 | 1.7 | 401.5 | 1.1 | 418.7 | 1.2 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 33,284.3 | 100.0 | 35,824.7 | 100.0 | 35,540.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.7.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Mac-25 Kiasi | Mac-25 Mchango (%) | Feb-26[r] Kiasi | Feb-26[r] Mchango (%) | Mac-26[p] Kiasi | Mac-26[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,634.0 | 56.0 | 20,773.0 | 58.0 | 20,543.5 | 57.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,602.0 | 55.9 | 20,750.0 | 57.9 | 20,520.8 | 57.7 |
| Malimbikizo ya riba | 32.0 | 0.1 | 22.9 | 0.1 | 22.7 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,405.1 | 4.2 | 1,581.5 | 4.4 | 1,551.5 | 4.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,327.6 | 4.0 | 1,501.2 | 4.2 | 1,471.6 | 4.1 |
| Malimbikizo ya riba | 77.5 | 0.2 | 80.2 | 0.2 | 80.0 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 12,117.8 | 36.4 | 12,741.7 | 35.6 | 12,717.2 | 35.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,744.3 | 35.3 | 12,416.8 | 34.7 | 12,376.5 | 34.8 |
| Malimbikizo ya riba | 373.5 | 1.1 | 324.9 | 0.9 | 340.6 | 1.0 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,127.4 | 3.4 | 728.6 | 2.0 | 728.0 | 2.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 953.9 | 2.9 | 675.0 | 1.9 | 672.7 | 1.9 |
| Malimbikizo ya riba | 173.5 | 0.5 | 53.6 | 0.1 | 55.4 | 0.2 |
| Jumla ya deni la nje | 33,284.3 | 100.0 | 35,824.7 | 100.0 | 35,540.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.7.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia**

| Shughuli ya uchumi | Mac-25 | Feb-26[r] | Mac-26[p] |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 20.7 | 22.5 | 22.5 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.4 | 22.0 | 22.0 |
| Kilimo | 4.9 | 5.3 | 5.3 |
| Nishati na madini | 13.1 | 12.0 | 12.0 |
| Viwanda | 3.6 | 3.7 | 3.7 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.0 | 19.4 | 19.2 |
| Fedha na bima | 4.4 | 3.6 | 3.6 |
| Utalii | 1.8 | 1.8 | 1.8 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 4.7 | 4.9 | 5.1 |
| Mengineyo | 5.5 | 4.8 | 4.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali.

**Jedwali 2.7.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia**

| Sarafu | Mac-25 | Feb-26[r] | Mac-26[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.3 | 66.0 | 66.7 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.9 | 17.7 | 17.7 |
| Yuan ya China | 6.3 | 6.5 | 6.6 |
| Sarafu nyinginezo | 9.5 | 9.7 | 9.0 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 38,447.9 mwisho wa mwezi Machi 2026, pungufu kidogo likilinganishwa na mwezi uliopita (Kielelezo 2.7.1). Deni litokanalo na hati fungani liliendelea kushika sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali, huku benki za biashara na mifuko ya hifadhi ya jamii zikiendelea kuwa wadai wakuu—zikimiliki zaidi ya nusu ya deni lote (Jedwali 2.7.5 na Jedwali 2.7.6).

**Kielelezo 2.7.1: Deni la ndani la Serikali kuu**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

**Jedwali 2.7.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo**

Shilingi Bilioni

| | Mac-25 | | Feb-26 | | Mac-26[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyenzo | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 29,313.2 | 85.6 | 33,122.0 | 85.4 | 33,321.1 | 86.7 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 1,888.8 | 5.5 | 1,653.0 | 4.3 | 1,575.3 | 4.1 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.5 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 27,237.2 | 79.5 | 31,333.2 | 80.8 | 31,609.9 | 82.2 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 4,942.2 | 14.4 | 5,659.7 | 14.6 | 5,126.8 | 13.3 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 4,923.9 | 14.4 | 5,659.6 | 14.6 | 5,126.8 | 13.3 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,255.4 | 100.0 | 38,781.7 | 100.0 | 38,447.9 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.7.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| | Mac-25 | | Feb-26 | | Mac-26[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Amount | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,948.4 | 29.0 | 10,834.3 | 27.9 | 10,925.8 | 28.4 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 6,883.9 | 20.1 | 7,468.4 | 19.3 | 6,935.5 | 18.0 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,091.5 | 26.5 | 10,463.9 | 27.0 | 10,463.9 | 27.2 |
| Kampuni za bima | 1,845.5 | 5.4 | 1,983.5 | 5.1 | 1,997.1 | 5.2 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 555.7 | 1.6 | 757.8 | 2.0 | 788.4 | 2.1 |
| Wengine | 5,930.3 | 17.3 | 7,273.8 | 18.8 | 7,337.0 | 19.1 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,255.4 | 100.0 | 38,781.7 | 100.0 | 38,447.9 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Mwezi Machi 2026, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 419 kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana za Serikali. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 276.7 zilikopwa kupitia uuzaji wa hati fungani na kiasi kilichobaki kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali za muda mfupi (Kielelezo 2.7.2). Malipo ya deni yalikuwa shilingi bilioni 518.2, yakijumuisha shilingi bilioni 219.9 zilizotumika kulipa deni la msingi na shilingi bilioni 298.3 kwa malipo ya riba.

**Kielelezo 2.7.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.8 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Mwenendo wa sekta ya nje ulionesha mwelekeo wa kupungua baada ya kipindi kirefu cha kuimarika, kama ilivyoashiriwa na ongezeko la nakisi ya malipo hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,492.5 mwishoni mwa mwezi Machi 2026, kutoka dola za Marekani milioni 2,009.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.8.1). Kwa kiasi kikubwa, ongezeko hili lilichangiwa na kasi kikubwa na uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususani bidhaa za viwandani na bidhaa za mitaji, ambao ulizidi kasi ya ukuaji wa mauzo ya nje.

Licha ya ongezeko la nakisi ya urari wa malipo, akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha ikifikia dola za Marekani milioni 6,084.4 mwishoni mwa mwezi Machi 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,693.2 mwishoni mwa mwezi Machi 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya nje pamoja na utekelezaji wa mpango wa Benki wa ununuzi wa dhahabu. Kiwango hicho kilitosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.7 ya makadirio ya uagizaji, na hivyo kubaki juu ya lengo la kitaifa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) (Kielelezo 2.8.1).

**Jedwali 2.8.1 Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali**

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Machi | | | Mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mar-26 | Feb-26 | Mar-26 | 2024 | 2025 | 2026^p | ya asilimia |
| Urari wa bidhaa | -318.9 | -341.5 | -762.8 | -6,049.5 | -4,524.9 | -4,891.3 | 8.1 |
| Zilozouzwa nje* | 713.6 | 1,070.1 | 815.0 | 7,718.5 | 9,593.2 | 11,076.9 | 15.5 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,032.6 | 1,411.6 | 1,577.8 | 13,768.0 | 14,118.1 | 15,968.2 | 13.1 |
| Urari wa huduma | 242.67 | 329.8 | 190.3 | 4,093.2 | 3,972.0 | 4,121.0 | 3.8 |
| Mapato | 513.6 | 627.0 | 494.7 | 6,390.8 | 6,905.0 | 7,526.6 | 9.0 |
| Malipo | 271.0 | 297.2 | 304.3 | 2,297.6 | 2,933.0 | 3,405.6 | 16.1 |
| Urari wa bidhaa na huduma | -76.3 | -11.7 | -572.5 | -1,956.3 | -552.9 | -770.3 | 39.3 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,227.2 | 1,697.1 | 1,309.7 | 14,109.3 | 16,498.2 | 18,603.5 | 12.8 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,303.5 | 1,708.8 | 1,882.1 | 16,065.6 | 17,051.1 | 19,373.8 | 13.6 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -167.6 | -220.0 | -214.8 | -1,583.9 | -1,987.5 | -2,181.5 | 9.8 |
| Yaliyoingia | 16.6 | 17.7 | 23.7 | 331.8 | 308.0 | 294.9 | -4.2 |
| Yaliyotoka | 184.2 | 237.7 | 238.5 | 1,915.7 | 2,295.6 | 2,476.5 | 7.9 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 27.0 | 14.8 | 13.5 | 698.2 | 530.5 | 271.7 | -48.8 |
| Iliyoingia | 82.9 | 74.0 | 74.2 | 1,334.1 | 1,118.4 | 917.2 | -18.0 |
| ambapo Serikali | 1.2 | 0.0 | 0.0 | 142.0 | 128.2 | 51.1 | -60.2 |
| Iliyotoka | 56.0 | 59.2 | 60.8 | 635.8 | 587.9 | 645.5 | 9.8 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -216.9 | -216.9 | -773.8 | -2,842.0 | -2,009.9 | -2,680.1 | 33.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.8.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Mauzo ya nje

